# JARIDA LA ACT

**TOLEO NA. 41**|SEPT–DES 2021

**Tunaunganisha, Shawishi na Kutetea**

## Wajumbe wa Bodi

Dkt. Jacqueline Mkindi- M/kiti
Mhe. Jitu Soni- Makamu M/kiti
Dkt. Sinare Y. Sinare -Mjumbe
Bw. Fabian Mwkatuma- Mjumbe
Bw. Enock Ndodole- Mjumbe
Bw. Zubery Mwachulla –Mjumbe
Bw. Omary Mwaimu – Mjumbe
Bw. Joeseph Masimba- Mjumbe
Bibi. Elde Kimaro- Mjumbe
Bw.. Abel Lyimo-Mjumbe

## Yaliyomo:

Mkutano wa Wadau wa Viungo

Warsha ya Kitaifa Kwenye Kilimo

Changamoto za Wadau wa Sekta Binafsi nchini Zajadiliwa

Kongamano la EAFF

Mkutano wa Wadau wa FO4ACP

Mafunzo ya kilimo shadidi kwa wakulima Wilayani MvomeroMkutano wa Wadau wa mnyororo wa thamani wa Kuku

Kongamano la Fursa ya Kibiashara (Tanzania – USA)

**ACT**

**JARIDA**
**Sept-Des 2021**

## MKUTANO WA WADAU WA VIUNGO WAFANYIKA

ACT ilishiriki Kongamano la Kitaifa la Viungo lililofanyika Masai Sunset Beach Resort, Chake Chake- Pemba. Mkutano huo ulifanyika tarehe 7 na 8 Desemba 2021 na uliratibiwa na AGRI-CONNECT (Mradi Unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya). Kaulimbiu ya mkutano ilikuwa ni "***Ufufuaji na Upanuzi wa Sekta ya Viungo Tanzania; Kukidhi Soko la Kimataifa"*** Mkutano ulihitimishwa kwa maaziimio yafuatayo;-

i. Kuimarisha na kuwezesha taasisi zinazosimamia maendeleo ya sekta ya viungo nchini,

ii. Kuimarisha eneo la utafiti, usindikaji, na huduma za ugani kwa maendeleo ya tasnia ya viungo,

iii. Kuoanisha Mkakati wa Maendeleo ya Viungo (Tanzania Bara na Zanzibar),

iv. Kuimarisha benki za viini (Germplasm bank) hasa katika Taasisi ya Udhibiti wa Viuatilifu (TPRI) na Shirika la Utafiti katika mimea ya asili ya mbogamboga na matunda (World Vegetable Center)

ACT iliwakilishwa na Bw. Khalid Ngassa, Meneja Huduma kwa Wanachama na Mawasiliano



# UZINDUZI WA MJADALA WA CHANGAMOTO ZA WADAU WA SEKTA BINAFSI NCHINI

Septemba 8, 2021, Baraza la Kilimo Tanzania kupitia Mkurugenzi Mtendaji ilishiriki katika kikao kilichoitishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapatao Tanzania (TRA) - Dar es Salaam kupitia taasisi ya Sekta Binafsi Nchini (TPSF). Mkutano huo, ulijadili na kubadilishana ufahamu kuhusu masuala yanayohusiana na kodi, na uboreshaji wa mazingira ya kibiashara. Miongoni mwa masuala yaliyowasilishwa na Baraza la Kilimo Tanzania ni pamoja na;

1. **Tume ya Maboresho ya Kodi (Tax Reform Commission)**

   Baraza la Kilimo Tanzania, limeiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania kuishawishi Wizara ya Fedha kuwa na wajumbe wa Sekta ya Kilimo kwenye Tume ya Maboresho

2. **Maboresho ya Kisera ya Muda Mrefu (Long Term Fiscal Policy Reform)**

   Baraza la Kilimo Tanzania, limeshauri kufanyika maboresho ya kisera ya muda mrefu kwa lengo la kulinda wakulima na viwanda vyetu. Endapo, maboresho hayo yatakuwa ya muda mrefu yatasaidia kuvuta wawekezaji kwa wingi nchini; tofauti na sasa, ambapo maboresho hufanyika mwaka mmoja mmoja.

3. **Makadirio Makubwa ya Kodi (Uplifting)**

   Baraza la Kilimo Tanzania, limependekeza kupitia utaratibu unaotumika kukadiria kodi kwa baadhi ya vifaa vya kilimo. Mantiki ni kulipa kodi kadri unavyonunua.

4. **Ushuru wa Zuio (Withholding Tax)**

   Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali ilielekeza ushuru wa zuio inapaswa kulipwa na kampuni na sio mkulima. Baraza la Kilimo Tanzania, limefatilia suala hili na kubaini kwamba wakulima bado wanaendelea kutozwa. Hivyo, kuna haja ya mamlaka husika kuvalia njuga suala hili.

# WARSHA YA KITAIFA YA KUTENGENEZA AGENDA YA UTAFITI KWENYE KILIMO (NARA)

Tarehe 29 na 30 Septemba 2021, ACT ilishiriki kongamano la siku mbili la wadau wa kutengeneza Agenda ya Kitaifa ya Utafiti kwenye Kilimo (NARA) kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (2022-2026). Kongamano hilo liliandaliwa na Wizara ya Kilimo kupitia taasisi ya utafiti kwenye Kilimo (TARI) na lilifanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Mipango-Dodoma. ACT ilikuwa sehemu ya kikosi kazi kilichotengeneza Agenda hiyo.

# KONGAMANO LA EAFF

Tarehe 13 na 14 Oktoba 2021, wajumbe wapatao 200 walihudhuria kongamano la Shirikisho la Vyama vya Wakulima vya Afrika Mashariki – EAFF kwa njia ya masafa (mtandao). Kongamano la aina hiyo hufanyika kila baada ya miaka minne. Taasisi zilizoshiriki kutoka Tanzania ni MVIWATA, TFC na ACT. Kaulimbiu ya kongamano hilo lilikuwa: **"Ushirikishwaji katika Uzalishaji: Soko la Ushindani, Uthabiti, na Matumizi ya Kidijitali kwa Maendeleo: Wakulima Wamejiandaaje?"** .Washiriki walijadili masuala hayo kwa kina na kukubaliana kwamba ili kufanikisha mapinduzi chanya, wanachama wa Shirikisho hili wanahitaji: dira, sera nzuri, elimu, ubunifu na ubia. Kongamano hilo lilikuwa na ajenda zifuatazo: i. kupokea taarifa ya utendaji; ii. kujenga jukwaa la mahusiano kati ya EAFF na Mashirika mengine, pamoja na sekta binafsi; iii. kuchagua Wajumbe wa Baraza na Bodi kwa muhula mpya. Katika uchaguzi huo, Bw. Omary Mwaimu kutoka ACT alichaguliwa kuwa Mjumbe kwenye Baraza.

# WARSHA YA WADAU WA MRADI WA FO4ACP

Tarehe 07 Oktoba 2021 ACT na washirika wake, iliandaa warsha ya wadau wa mradi wa FO4CAP uliyofanyika jijini Arusha, kujadili masuala yaliyoibuliwa wakati wa kutekeleza mradi huo, mafanikio yake, na mipango ya baadae. Wadau kama ACT, TAHA, MVIWATA, MVIWA Arusha, MVIWA Manyara, Tanzania Federation of Cooperatives (TFC), Food and Forest Development Finland (FFD), AHA, TRIAS na We Effect walishiriki. Wajumbe wa mkutano, walishuhudia utiliwaji saini (Makubaliano - MoU) kwa lengo la kuratibu shughuli za mradi katika ngazi ya kitaifa baina ya Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) na AgriCord Alliance kwa niaba ya washirika wake. Mradi wa FO4ACP unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) kupitia Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD). Lengo kuu la Mradi ni kuongeza mapato na kuboresha maisha, usalama wa chakula na lishe, na usalama wa wakulima wadogo katika nchi za Kiafrika, Karibiani na Pasifiki.



Washiriki wa warsha ya wadau wa FO4ACP - Ofisi za TAHA, Arusha

# MAFUNZO YA KILIMO SHADIDI KWA WAKULIMA WA WILAYA YA MVOMERO

Kuanzia tarehe 02 mpaka 05 Novemba, 2021, Afisa Mradi kutoka ACT-Bw. Obedi Abraham na Mshauri Elekezi Bw. Hendry Mziray waliendesha mafunzo ya siku tano kuhusu Kilimo Shadidi na matumizi bora ya viuatilifu kwa wakulima wa Wilaya ya Mvomero-Mkoani Morogoro katika Skimu za Umwagiliaji,- Mkindo na Dakawa. Mafunzo yalihudhuriwa na washiriki 110 ikijumuisha; Maafisa Ugani, wakulima viongozi, wauzaji wa pembejeo n.k. Mradi wa SFOAP ni wa miaka mitano (2019-2023) unafadhiliwa na Shirikisho la Wakulma Kusini mwa Afrika (SACAU) na umelenga kuwafikia wakulima wadogo wapatao 16,000 wakiwemo wanawake na vijana katika Wilaya ya Mvomero kwa kuwapa mafunzo kwenye kilimo shadidi na hifadhi.



**Mkufunzi akitoa somo kuhusu kilimo shadidi Dakawa, Morogoro.**

# MKUTANO WA WADAU WA MNYORORO WA THAMANI WA KUKU

Desemba 10 2021, ACT iliendesha warsha kuhusu ushiriki wa vijana katika mnyororo wa thamani wa kuku iliyofanyika katika Hoteli ya Golden Park iliyopo Dar es Salaam-Tanzania. Mkurugenzi Mtendaji wa Baraza la Kilimo, Bw. Timoth Mmbaga alifafanua lengo la warsha ni kujadili matokeo ya utafiti kuhusu "Kiwango cha Ushirikishwaji wa Vijana katika Mnyororo wa Thamani kwenye tasnia ndogo ya Kuku nchini Tanzania". Utafiti huo ulifanywa na mtalaam elekezi kutoka kampuni ya AB Consult Bw. Joseph Longo, takribani vijana 40 wanaojihusisha na Mnyororo wa Thamani kwenye kuku; wazalishaji, madawa na utoaji wa huduma, uuzaji wa vifaa, usindikaji na ufungashaji wa bidhaa za kuku walihudhuria. Utafiti huo ulifadhiliwa na Shirikisho la Vyama vya Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU) kupitia mradi wa SFOAP. SACAU na ACT inakusudia kuandaa jukwaa la kikanda ambalo litaunganisha vijana katika mnyororo wa thamani wa kuku katika nchi za SADC kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kutengeneza mahusiano ya kibiashara. Usajili kwenye jukwaa unpatikana kupitia http://survey.actanzania.or.tz



**Picha ya Pamoja: Washiriki wa Mkutano wa mnyororo wa thamani wa Kuku**



**Mkurugenzi wa Miradi kutoka ACT (Bw. Mark Magila) akifunga warsha ya wadau wa kuku**

## KONGAMANO LA FURS YA KIBIASHARA LAFANYIKA

Tarehe 7 Desemba 2021, Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) kwa kushirikiana na taasisi ya Sister Cities International Region Africa (Tanzania Sister Cities), Southern Agricultural Growth Corridors of Tanzania (SAGCOT) Ltd, Thunderbird School of Global Management - kutoka Chuo Kikuu cha Arizona State, na Ubalozi. wa Tanzania nchini Marekani waliandaa Kongamano la Kilimo Biashara kwa lengo la kufanya biashara kupitia utaratibu wa AGOA. Kongamano hilo, lililenga kuzitayarisha na kuziwezesha Sekta Binafsi nchini Tanzania  na Marekani kwa kuzijengea uwezo katika uagizaji na uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi kupitia AGOA. Katika kipindi cha miezi 12 ijayo, Ubalozi wa Tanzania nchini Marekani utaendesha mfululizo wa makongamano ya kibiashara ya aina hiyo.

**Tunaunganisha, Shawishi na Kutetea**

## Dira na Dhamira ya ACT

**DIRA**

Kuwa na Sekta ya Kilimo iliyofanikiwa, endelevu na shindani: inayohakikisha usalama wa chakula na lishe unaotokana na msukumo wa kisekta binafsi
.

**DHAMIRA**

Kutetea, kuratibu na kuwezesha mazingira rafiki kwa kilimo-biashara

## Malengo ya ACT

- Kujenga mazingira wezeshi kwa kilimo-biashara
- Kujengea uwezo wanachama wa ACT katika utoaji wa huduma
- Kutuma na kupokea taarifa kutoka wanachama na wadau wengine zinazohusu ustaw wa Sekta ya Kilimo nchini.
- Kuratibu na kuendesha mashirikiano katika ngazi ya taifa na wilaya
- Kuratibu jitihada za Sekta ya Umma na Binafsi katika uendelezaji wa Kilimo biashara


## *Bodi ya Uhariri*

1. ***Mr. Timoth Mmbaga - Mwenyekiti***
2. ***Mr. Mark Magila- Mjumbe***
3. ***Ms. Laetitia William - Mjumbe***
4. ***Mr. Khalid Ngassa- Mjumbe***
5. ***Mrs. Susan Masagasi- Mjumbe***



## Wasiliana Na.

Mkurugenzi Mtendaji
Agricultural Council of Tanzania
S.L.P 14130,
Dar es
Salaam.

**Simu:** +255 22 2761344,
**Nukushi:** +255 22 2128032
**Barua pepe:** act@actanzania.or.tz
**Tovuti:** www.actanzania.or.tz


# Hii ndiyo PFS

***Ubia wa Mradi wa PFS"*** unaratibu na kuwezesha watendaji mbalimbali kwenye mnyororo wa thamani wa wadau chini ya mfumo wa mashirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP). Mradi unatekelezwa na Baraza la Kilimo Tanzania (ACT). Lengo lake ni kuchangia na kuongeza kiwango cha mafanikio yaliyopatikana kwenye awamu ya pili ya Mradi wa Ubia wa Kilimo Tanzania (TAP II) katika kipindi cha Oktoba 2014 had Mei 2020. Mradi huo ulifanikiwa ukuaji wa kilimo kwa kutumia mbinu za kilimo biashara na uwekezaji.

### Malengo ya Mradi

**Lengo kuu ni;**Kuongeza usalama wa chakula na lishe, na kupunguza umasikini. Umaskini unatarajiwa kupungua kwa 17%, halikadhalika na ukosefu wa lishe kwa watoto kupungua kwa 5%.

### Utaratibu wa Utekelezaji

Mradi utatumia mbinu ya ubia katika utekelezaji wa mradi. Mradi wa PFS, chini ya Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) utaratibu na kuongeza uwezeshaji na utekelezaji ili kuhakikisha ubia unaimarishwa na mafanikio tarajiwa yanafikiwa. Mradi unatumia ujuzi na maarifa ili kutatua vikwazo muhimu kwenye mnyororo wa thamani. Mradi umeainisha Asasi za Kiraia 35, wabia kutoka setka ya umma na binafsi (ndani na nje ya nchi), wenye uwezo na majukumu mbalimbali watakaoshirikishwa katika kazi ya ubia


**Kwa taarifa zaidi, wasiliana na:**
Mratibu Taifa
Mradi wa PFS
S.L.P 14130, Dar es Salaam Email:
act@actanzania.or.tz
Tovuti:www.actanzania.or.tz


**PFS inawajibika kwa Bodi ya Wakurugenzi wa ACT**